

**HALMASHAURI YA JIJI DODOMA**  
**MAZOEZI YA LIKIZO SOMO LA MAARIFA YA JAMII**

**SEHEMU A: Chagua jibu sahihi**

1. (i) Kazi kubwa ya kamati ya shule ni \_\_\_\_\_  
 (a) Kusajili wanafunzi      (c) kuajiri waalimu  
 (b) Kuadhibu wanafunzi      (d) kusimamia maendeleo ya shule      ( )
- (ii) Uwezo wa mtu kukabili changamoto mbalimbali huitwa \_\_\_\_\_  
 (a) Ujasiri (b) Ushirikiano (c) Taaluma (d) Nidhamu      ( )
- (iii) Zifuatazo ni tabia hatarishi kwa watoto ISIPOKUWA:  
 (a) Kucheza barabarani (b) Kushirikiana na wengine katika masomo  
 (c) Kurushia mawe mbwa na mizinga ya nyuki  
 (d) Kukubali zawadi kwa mtu usiyemfahamu
- (iv) Picha ya kiongozi yupi kati ya hawa wafuatao huonekana kwenye sarafu ya shilingi miatano ya fedha za Kitanzania?  
 (a) Mwalimu Julius K. Nyerere (b) Ali Hassan Mwinyi (c) Rashid Mfaume Kawawa (d) Sheikh Abeid Amani Karume
- (v) Miiongoni mwa njia za kutunza mazingira yetu ni pamoja na:  
 (a) Kutupa takataka baharini, ziwani au mtoni (b) Kukata miti yote Inayotuzunguka (c) Kupanda miti katika maeneo yanayotuzunguka  
 (d) Kutumia mbolea za viwandani katika kilimo

**2. Oanisha kifungu cha maneno katika sehemu A na sehemu B kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku kilichoachwa wazi hapo chini**

	<b>SEHEMU A</b>	<b>JIBU</b>	<b>SEHEMU B</b>
i	Vitu ambavyo vinaweza kuleta utajiri kwa mtu, familia au Taifa		A. Kipaji
ii	Uwezo wa kutenda jambo jema kwa ustadi		B. Upandaji miti
iii	Kitu au jambo linaloweza kukwamisha kufikia malengo uliyojiwekea		C. Sindimba
iv	Moja ya njia zinazotumika katika utunzaji wa mazingira		D. Rasilimali
v	Ngoma ya asili ya wamakonde		E. Changamoto
			F. NEMC
			G. Uzalishaji

**3. Jibu swali la (11-15) kwa kubainisha vitendo vya usaliti au vitendo vya uwazi na uaminifu kwa kuweka alama ya tiki ( ✓ ) katika sehemu sahihi**

	Matendo	Matendo ya usaliti	Matendo ya uwazi na uaminifu
Mfano	kusaidia wengine		✓
i	Kusema uwongo		
ii	Uaminifu		
iii	Kukubali makosa		
iv	Kutokuwa mwaminifu		
V	Kusengenya		

**4: Andika NDIYO au HAPANA**

- i. B. O. T ni Benki kuu ya Tanzania \_\_\_\_\_
- ii. 9/12/1961 bendera ya Taifa ilipeperushwa katika cha mlima Kilimanjaro \_\_\_\_\_
- iii. Kitendo cha mtu kuipenda nchi yake na kuwa tayari kuitetea kinaitwa uzalendo \_\_\_\_\_
- iv. Wimbo wa Taifa si wimbo maalumu wa nchi huru \_\_\_\_\_
- v. Matumizi ya kuni hushauriwa katika utunzaji mazingira \_\_\_\_\_

**Tazama kwa makini picha i fuatayo kasha jibu swali linalofuatia:**



(i) Alama inayoonekana katika picha hapo juu huwakilisha\_\_\_\_ na Amani miongoni mwa Watanzania.

### **1. Soma majigambo yafuatayo kisha jibu maswali yanayofuata**

**Mwalimu mkuu:** Mimi ndiye kiongozi mkuu wa shule. Ninasimamia shughuli zote za kiutawala shulenii. Walimu wote hupokea maagizo kutoka kwangu. Mimi pia ni katibu wa Kamati ya shule.

**Mwalimu mkuu msaidizi:** Kama jina la cheo changu lilivyo, mimi ni msaidizi wa Mwalimu Mkuu. Ninamshauri Mwalimu mkuu juu ya namna bora ya kuongoza shule. Mwalimu mkuu asipokuwepo kazini mimi ndiye ninayetimiza majukumu yake.

**Mwalimu wa taaluma:** Mimi ni mtu muhimu sana shulenii. Ninasimamia masuala yanayohusu taaluma shulenii. Ninawapangia vipindi vya masomo walimu wengine na kufuatilia namna ya ufundishaji wao. Vilevile mimi ndiye ninayeandaa ratiba ya ufundishaji shulenii.

**Mwalimu wa nidhamu:** Mimi ndiye msimamizi mkuu wa masuala yahusuyo nidhamu kwa wanafunzi. Ninahakikisha kwamba sheria na kanuni zote za shule zinafuatwa na kila mwanafunzi. Pasipo mimi wanafunzi hawawezi kuwa na tabia njema.

### **MASWALI**

- i. Nani anayehusika na masuala ya kila siku ya utawala Mwalimu mkuu asipokuwepo shulenii?\_\_\_\_\_

- ii. Nani anayehusika na kuandaa ratiba ya shule na kugawa majukumu ya ufundishaji kwa walimu? \_\_\_\_\_
- iii. Ni Mwalimu gani anahuusika na usimamizi wa tabia za wanafunzi shulenii? \_\_\_\_\_
- iv. Kiongozi mkuu wa shule ni nani? \_\_\_\_\_